Swahili

PARENT NETWORK OF WESTERN NEW YORK

716.332.4170
info@parentnetworkwny.org

Kusaidia · Kuelimisha · Kuunganisha · Kuwezesha

Tunasaidia familia na wataalamu ambao huwawezesha watu binafsi wenye ulemavu kufikia uwezo wao kamilikupitia elimu na nyenzo.

Tunaelewa mahitaji ya familia kwa kila hatua ya ukuaji; kutoka utotoni na umri wa kwenda shule, hadi utu uzima.



Utotoni

Umri wa Kwenda Shule

Utu Uzima

parentnetworkwny.org

ParentNetwork PNWNY

Tuko hapa katika kila hatua, kuzisaidia familia na wataalamu.

USAIDIZI WA ANA KWA ANA

Familia na wataalamu wanahimizwa kuwasiliana na mmoja wa wataalamu wetu waliopokea mafunzo ili kutumia mifumo na kuunganishwa na nyenzo. Huduma ya ukalimani wa bila malipo ipo kwa watu wasiozungumza Kiingereza.

HUDUMA ZA USAIDIZI WA FAMILIA

Wataalamu wetu wa Usaidizi wa Familia wataelimisha na kushirikisha familia za watu binafsi wenye ulemavu katika vikundi vidogo au ana kwa ana.

USAIDIZI WA USTAHIKI

Mwelekezi wetu wa Ustahiki anaweza kuzisaidia familia katika Kaunti ya Erie au ya Niagara kujaza hati zinazohitajika ili kuanzisha mchakato wa ustahiki wa Ofisi ya Watu Wenye Ulemavu wa Ukuaji (OPWDD).

USAIDIZI WA TABIA

Mtaalamu wetu wa Tabia anashirikiana na familia katika Kaunti ya Erie au ya Niagara ambazo wana watoto wanaoishi nyumbani na wanastahiki huduma za OPWDD.

WARSHA NA HAFLA

Tunaandaa warsha za mtandaoni na za ana kwa ana ili kuwasaidia wanafamilia, watu binafsi na wataalamu kuelewa vyema ulemavu na kuongeza ujuzi wao wa elimu maalum na mifumo ya usaidizi.

NYENZO ZA MTANDAONI



Tovuti yetu huipa jumuiya yetu maelezo na nyenzo kuhusu hafla zijazo, warsha, laha za maelezo na video zinazoweza kupakuliwa.

PARENT NETWORK
OF WESTERN NEW YORK